JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Boma Road,
S.L.P. 484,
SINGIDA,
Barua Pepe: rbcsingida@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

SINGIDA – JULAI 15, 2019

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA SINGIDA YAWAFIKISHA MAHAKAMANI WATENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA NA MHASIBU WIZARA YA AFYA KWA UHUJUMU UCHUMI

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU ni chombo chenye dhamana ya kusimamia Mapambano Dhidi ya Rushwa nchini tukiongozwa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni TAKUKURU Mkoa wa SINGIDA ambayo inajumuisha H/MANISPAA SINGIDA pamoja na Wilaya za IRAMBA, MKALAMA,ITIGI IKUNGI, MANYONI na SINGIDA vijijini imeweza kutekeleza majukumu yake kwa kufanya kazi zifuatazo kama sehemu ya mpango wa utekelezaji wa majukumu yake.

1. UCHUNGUZI

a) Ka tika dawati la uchunguzi jumla ya Taarifa 85 zimepokelewa zinazohusu idara mbalimbali kama ifuatavyo:, Halmashauri 26, Ardhi 10 , Mahakama 12, Polisi 13 Afya 09, Elimu 03, fedha 02, Biashara 02, Ushirika 02,Maji 03, Siasa 02 na Binafsi 01. Kupitia taarifa hizo Idara zinazoongoza kwa kulalamikiwa na wananchi zaidi kujihusisha na vitendo vya rushwa ni pamoja na Halimashauri za wilaya , Polisi , Mahakama, Idara ya ardhi ,Elimu na Maji. Chunguzi mbalimbali dhidi ya tuhuma husika zinaendelea.

b) Aidha kupitia uchunguzi tumeweza kuokoa fedha kiasi cha Tshs**. 40,000,000.00/=** ambazozingeliwa na wala rushwa, zimeokolewa na fedha hizo zipo kwenye akaunti ya HAZINA (BOT) .

c) Jumla ya kesi mpya Kumi na Mbili (12) zilifikishwa mahakamani kwa kipindi hicho na kesi zinazoendelea mahakamani hadi hivi sasa ni nane (08). Na kesi nyingine nne (04) zilishinda mahakamani .Kesi hizo zinahusisha idara za Ardhi ,Jeshi na Elimu .

Moja ya kesi iliyofikiwa mahakamani mnamo 23/05/2019 ni ya watuhumiwa watatu ambao ni Mfamasia wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ndugu ELIKANA LUBANGO ISANZU, Afisa Chanjo wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ndugu EMMANUEL ALEXANDER MAWI na Mhasibu wa Wizara ya Afya ndugu BITA

MAGAI HITLER kwa makosa ya Matumizi Mabaya ya Mamlaka, Ubadhirifu na Ufujaji wa fedha na Kuisababishia Hasara Serikali ya shilingi milioni 14, 660,000/=.

2. UELIMISHAJI

Kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa TAKUKURU kupitia Idara ya Elimu kwa Umma hutumia mbinu mbalimbali kuwaelimisha na kuwashirikisha wanajamii wa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vijana wa shule za msingi,sekondari na vyuo. Pia Ili kuwafikia na kuwaelimisha walengwa TAKUKURU inashirikiana na wadau wengine wa mapambano dhidi ya rushwa ambao ni pamoja na Taasisi za dini, mashirika ya Umma, mashirika yasiyo ya serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi. Elimu kwa Umma ilitolewa kwa makundi mbali mbali katika jamii ambapo jumla ya klabu katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo zilizoelimishwa na kuimarishwa zilikuwa 20, Semina kwa Idara mbalimbali na watendaji vijiji na mitaa , vituo vya afya 13 na mikutano ya hadhara iliyotolewa kwa wananchi ilikuwa 8.

3. UDHIBITI

Ili kudhibiti mianya ya rushwa katika Idara mbalimbali TAKUKURU (M) SINGIDA imefanya kazi ya kubaini mifumo yenye mianya ya rushwa kwa kufanya uchambuzi wa mifumo kubaini mapungufu, kufanya warsha na idara husika na kisha kufanya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio yaliyotolewa. Mifumo Sita (06) ilifuatiliwa ambayo ni ukusanyaji wa kodi ya majengo na udhibiti wa mianya ya rushwa katika taratibu zinazotumika katika kujaza mafuta katika magari ya serikali Halmashauri ya Manispaa na H/W ya Singida

Pia uchambuzi wa mfumo kuhusu mfumo wa uendeshaji wa mabaraza ya ardhi ya kata wilaya ya Mkalama na uchambuzi wa mfumo kuhusu mapato yatokanayo na stand ya mabasi manyoni warsha tatu zilifanyika ambazo zilijumuhisha tasisi husika na Takukuru katika kubainisha mianya katika uchambuzi wa mfumo kuhusu utoaji wa mikopo kwa vijana ,wanawake na wenye ulemavu-h/wilaya Manyoni na H/w ya Itigi na kuweka maazimio ya kuziba mianya Rushwa.

4. MIRADI YA MAENDELEO

Lengo la kufanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ni pamoja na kujenga uelewa wa pamoja kuhusu kiasi cha pesa kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya ujenzi, ukarabati wa barabara,afya,elimu, maji n.k iliyopo chini ya Mamlaka za Serikali za mitaa,wakalaza serikali na serikali kuu, kufuatilia ili kuona uwiano kati ya matumizi ya fedha za umma na ubora wa huduma zinazotolewa,kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa utekelezaji wa bajeti, kuimarisha ufanisi na matokeo mazuri ya matumizi ya fedha za umma na kupata msingi wa kufanya udhibiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti katika miradi husika.

Miradi mbalimbali ilikaguliwa na TAKUKURU katika Mkoa wa Singida ikiwepo

Miradi ya afya mnne(4) yenye thamani ya bilioni 1.7 ,miradi ya maji tisa (9) yenye thamani bilioni 4.4, miradi ya elimu nane (8) yenye thamani ya bilioni 1.1 na mradi mmoja(1) wa barabara wenye thamani ya milioni 120/=. Jumla ya thamani ya miradi yote iliyokaguliwa ni bilioni 7.3 na katika miradi hiyo yote miradi inayochunguzwa ina thamani ya bilioni 1,116,174,000/=.

5. MKAKATI WA UTENDAJI KAZI KUANZIA JULAI – SEPTEMBA 2019

Mkakati wa utendaji kazi TAKUKURU (M) kwa robo mwaka ya kwanza inayoanzia JULAI hadi SEPTEMBA ni kuendelea kufanya Uchunguzi kwa taarifa zote za vitendo vya rushwa zitakazoibuliwa, kufanya uelimishaji kwa jamii kuhusiana na madhara ya rushwa hasa jwenye uchaguzi utakaokuja wa serikali za mitaa na pia uchaguzi mkuu wa 2020, ufuatiliaji kwa kina katika miradi ya maji, afya na elimu kwa lengo la kuona uwiano wa fedha zilizotolewa na serikali na majengo yanayojengwa au manunuzi ya vifaa.

TAKUKURU (M) inazidi inatoa rai kwa wananchi wote kwa ujumla kujiepusha na vitendo vya Rushwa na kushiriki kikamilifu kutoa taarifa za vitendo vya rushwa pale wanapobaini kutokea/kutaka kutokea kwa vitendo vya rushwa na kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi na kushiriki kutoa ushahidi mahakamani

Imetolewa na:

Signed

Joshua Msuya
Kaimu Mkuu wa TAKUKURU (M) Singida